

# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

## MRADI WA KUKUZA ELIMU NA UJUZI KWA KAZI ZENYE TIJA(ESPJ)

Anuani ya simu: "ELIMU"  
Simu: 026 296 35 33  
Email:info@moe.go.tz  
Tovuti: [www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz)  
*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb: Na.NYSDVTC/2019/2020/LOT3



Mji wa Serikari,  
Eneo la Mtumba  
Mtaa wa Afya,  
S. L. P. 10,  
40479 DODOMA.

Tarehe ya Tangazo: 16/09/2019

### TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MAFUNDI UJENZI (LOCAL FUNDIS)-UJENZI WA NYASA DVTC

Kwa kusudi la kuimarisha ujuzi kwa vitendo kwa wanafunzi wa fani mbalimbali za ufundi kuitia vyuo vya ufundi stadi (VETA) Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (WyEST) kuitia mradi wa kukuza elimu na ujuzi kwa kazi zenyetija(ESPJ) inatarajia kujenga vyuo mbalimbali vya ufundi stadi katika Halmashauri mbalimbali nchini.

Mradi huu unatekelezwa kwa mwongozo wa '*FORCE ACCOUNT*' wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuitia mtaalam elekezi ambaye ni Chuo cha Ufundi Arusha (*Arusha Technical College-ATC*) na kamati za miradi (*Project Committees*) katika Halmashauri husika ambapo mradi huu utatekelezwa kwa kushirikiana na Ofisi za' VETA' katika kanda za mikoa husika.

Moja kati ya Halmashauri ambazo mradi huu utatekelezwa ni Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, ambapo chuo kitajengwa eneo la Kilosa umbali wa taribani kilometra 3 (3km) kutoka Makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya.

Miundombinu inayotarajia kujengwa ni kama inavyooneshwaa katika jedwari hapa chini:

Jedwari la miundombinu inayotekegemea kujengwa.

NA.	AINA YA JENGU AU MIUNDOMBINU INAYOTARAJIA KUJENGWA	IDADI	MAELEZO
1	Jengo la Utawala (Administration Block)	01	Maelezo zaidi ya michoro yatatolewa
2	Jengo la bweni la wavulana na wasichana (Dormitories)	02	Maelezo zaidi ya michoro yatatolewa
3	Jengo la bwalo na jiko (Dining Hall and Kitchen)	01	Maelezo zaidi ya michoro yatatolewa
4	Jengo la madarasa mawili (2Classrooms Block)	01	Maelezo zaidi ya michoro yatatolewa
5	Majengo ya karakana (Workshops' Buildings)	05	Maelezo zaidi ya michoro yatatolewa
6	Jengo la vyoo vya nje (Ablution Blocks)	03	Maelezo zaidi ya michoro yatatolewa
7	Kibanda cha milanzi (Guard House)	01	Maelezo zaidi ya michoro yatatolewa
8	Banda litakalotumika wakati wa ujenzi(Camp site)+Stoo	01	Maelezo zaidi ya michoro yatatolewa
9	Nyumba ya mkuu wa Chuo na nyumba za walimu	03	Nyumba za walimu

10	Ujenzi wa Septic & Soakway pits	01	Maelezo zaidi ya michoro yatatolewa
11	Mfumo wa maji safi na maji taka(Water Supply & Sewage System)	-	Katika jengo husika na kutoka katika chanzo
12	Uwekajia wa mfumo wa umeme (Installation of Electrical System)	-	Katika jengo husika na kutoka katika chanzo

Hivyo Mwenyekiti wa kamati ya mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Ufundti stadi (VETA) katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa anawatangazia wananchi wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kufanya kazi tajwa hapo juu katika fani, sifa na masharti kama yaliyoahinishwa katika tangazo hili kuomba kazi katika fani zifuatzo:

#### I) FANI NA MASHARTI/SIFA MAHUSUSI ZA MAFUNDI ZINAZOHITAJIKA;

##### A. FUNDI UASHI NA KUPAUA (BOMA, KUPAUA, LIPU, SAKAFU NA RANGI).

- 1) Awe amewahi kufanya kazi inayofanana na kazi hii yenye thamani ya jumla ya gharama za ufundi isiyopungua Tshs. 15,000,000.00 (Kumi na tano Milioni).
- 2) Lazima aambatanishe mkataba wa kazi yenye thamani tajwa hapo juu na barua pendekezwa (recommendation letter) kutoka kwa Mwajiri wa awali aliyempa kazi hiyo.
- 3) Awe na uwezo wa kusoma michoro na kufanya makadirio ya mahitaji (materials).
- 4) Awe na uwezo wa kuseti msingi,kusuka nondo na kujenga kwa ufasaha.
- 5) Awe na uwezo wa kujenga kwa mawe, tofali zote za block na za kuchoma.
- 6) Awe na uwezo wa kupaua paa za aina mbalimbali katika majengo ya serikali.
- 7) Awe na uwezo wa kupaua mabati ya aina zote na kufanya '*blanderling & ceiling*'
- 8) Awe na uwezo wa kupiga lipu kuta.
- 9) Awe na uwezo wa kuweka sakafu za za aina mbalimbali (za kawaida,tiles,terrezo n.k).
- 10) Awe na uwezo wa kutumia mitambo na vifaa mbalimbali vyta ujenzi.
- 11) Awe na timu ya kutosha ya mafundi wasaidizi na vibarua wenye weledi wa kazi.
- 12) Fundi mmoja anaruhusiwa kuomba majengo yasiyozi mawili (2) tu kwa idadi.
- 13) Fundi atahesabika kuwa ameshinda baada ya kusahiliwa ufundi wake kwa maswali/vitendo(Technical Evaluation) na gharama za ufundi (Financial evaluation).
- 14) Michoro na fomu za mchanganuo wa shughuli za ujenzi za mradi huu zinapatikana katika Ofisi ya Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa.
- 15) Fundi lazima ajaze vipengele vyote vilivyoahinishwa katika fomu ya mchanganuo wa gharama za ujenzi kwa majengo na miundombinu mbalimbali.
- 16) Cheti cha ufundi ni sifa ya ziada kwa fundi husika.

## B. FUNDI UMEME

- 1) Awe amewahi kufanya kazi inayofanana na kazi hii yenyé thamani ya jumla ya gharama za ufundi isiyopungua Tshs. 5,000,000.00 (Tano Milioni).
- 2) Lazima aambatanishe mkataba wa kazi yenyé thamani tajwa hapo juu na barua pendekezwa (recommendation letter) kutoka kwa Mwajiri wa awali aliyempa kazi hiyo.
- 3) Awe na uwezo wa kusoma ramani/mchoro na kuitafsiri.
- 4) **Awe amesajiliwa na kupata Leseni kutoka Ewura**
- 5) Awe na uwezo wa kuweka mfumo wa kung' amua moto (fire detectors).
- 6) Awe na uzoefu wa kufunga umeme katika majengo ya serikali na mitambo/mashine.
- 7) Fundi atahesabika kuwa ameshinda baada ya kusahiliwa ufundi wake kwa maswali/vitendo(Technical Evaluation) na gharama za ufundi (Financial evaluation).
- 8) Michoro na fomu za mchanganuo wa shughuli za ujenzi za mradi huu zinapatikana katika Ofisi ya Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa.
- 9) Fundi lazima ajaze vipengele vyote vilivyoahinishwa katika fomu ya mchanganuo wa gharama za ujenzi kwa majengo na miundombinu mbalimbali.
- 10) Cheti cha ufundi ni sifa ya ziada kwa fundi husika

### C. FUNDI BOMBA

- 1) Awe amewahi kufanya kazi inayofanana na kazi hii yenyе thamani ya jumla ya gharama za ufundi isiyopungua Tshs. 7,500,000.00 (Saba Milioni Mia Tano Elfu).
- 2) Lazima aambatanishe mkataba wa kazi yenyе thamani tajwa hapo juu na barua pendekewza (recommendation letter) kutoka kwa Mwajiri wa awali aliyempa kazi hiyo.
- 3) Awe na uwezo wa kusoma michoro/ramani ya maji safi/taka na kuitafsiri
- 4) Awe na uwezo wa kufanya makadirio ya mahitaji (materials) ya mfumo wa maji.
- 5) Awe na uwezo wa kujenga/kutengeneza mfumo wa maji safi.
- 6) Awe na uwezo wa kujenga/kutengeneza mfumo wa maji taka uliokamilika utakayojuisha '*inspection chambers, septic & soak-way pits*'
- 7) Fundi atahesabika kuwa ameshinda baada ya kusahiliwa ufundi wake kwa maswali/vitendo(Technical Evaluation) na gharama za ufundi (Financial evaluation).
- 8) Michoro na fomu za mchanganuo wa shughuli za ujenzi za mradi huu zinapatikana katika Ofisi ya Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa.
- 9) Fundi lazima ajaze vipengele vyote vilivyoahinishwa katika fomu ya mchanganuo wa gharama za ujenzi kwa majengo na miundombinu mbalimbali.
- 10) Cheti cha ufundi ni sifa ya ziada kwa fundi husika

#### **II) MASHARTI YA UJUMLA KWA MWOMBaji;**

- 1) Mwombaji lazima awe raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18.
  - 2) Mwombaji lazima awe na Namba ya Utambulisho ya Mlipa Kodi (TIN number).
  - 3) Mwombaji lazima awe na Akaunti ya benki iliyo hai.
  - 4) Mwombaji lazima aandike barua ya maombi akiwa ameambatanisha nyaraka zote kama zilizotajwa katika tangazo hili pamoja na picha ndogo (passport size) mbili(2) za rangi.
  - 5) Kwa fundi ambaye anataka kuomba fani mbili tofauti atalazimika kutuma barua mbili (2) tofauti kw afani hizo.
  - 6) Maombi yatakayowasilishwa kwa njia ya FAX, Telefax, Telegraphic system na posta hayatapokelewa.
  - 7) Cheti ni sifa ya ziada kwa mwombaji.
  - 8) Mwombaji lazima aambatanishe barua ya mdhamini mwenye mali zisizohamishika na barua kutoka Ofisi ya Serikali ya Kijiji/mtaa.
  - 9) Mwombaji awe tayari kufanya kazi kwa awamu (shift) na siku za mwisho wa wiki itakapolazimika kufanya hivyo.
  - 10) Kazi ya ujenzi kwa mradi huu inatarajia kuchukua muda wa miezi mitatu (03).
  - 11) Barua za maombi yote yawasilishwe kwa njia ya mkono Ofisi ya Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi yakiwa yameandikwa anuani ifuatayo:  
Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi ya mradi wa Chuo cha cha VETA , S.L.P 51,Nyasa-Lindi 90  
Ru  
Tanzania.
  - 12) Mwisho wa kupokea Maombi ni tarehe 23/09/2019 saa 8.00 MCHANA
  - 13) Mafundi wote watataarifiwa (kwa njia ya simu) ili kufika siku ya tarehe ya usahili .

*Tangazo hili limeandalika na mtaalam elekezi wa mradi na kutolewa namwonyekiti wa kamati ya mradi:*

Meneja miradi,  
Chuo cha Ufundi Arusha(ATC)  
S.L.P . 296,  
Arusha – Tanzania

**ATC - PRODUCTION AND CONSULTING BUREAU**  
ARUSHA TECHNICAL COLLEGE  
P. O. Box 295, ARUSHA, TANZANIA  
Tel: +255 27 250 3040  
E-Mail: atpc@atc.ac.tz

Mwenyekiti,  
Kamati ya ujenzi ya mradi wa VETA,  
S.L.P ,90  
Nyasa – RuvumaTanzania  
Saini na muhuri au kimojawapo

*F. L'Heure*